

Swahili transcript:

Upendo: Ningependa pia kuzungumzia kuhusu utalii Tanzania. Aaah! Tunawakilisha utalii wetu Tanzania katika mambo mbalimbali. Kwa mfano, tuna mbuga za wanyama ambazo ni nyingi kwa kweli kwa Tanzania. Nikitolea mfano, tuna mbuga ya wanyama ya Serengeti, tuna mbuga ya wanyama ya Manyara, kuna Tarangire, kuna Mikumi, na mbuga nyingine nyingi tu. Sasa katika kuwaeleza dunia na ulimwengu kwa ujumla kwamba tuna mbuga za wanyama, mara nyingine tunatumia redio, tunatumia televisheni, tunatumia mitandao mbalimbali, kama internet. Lakini vilevile hata katika mavazi yetu; pia tunautangaza utalii Tanzania. Kwa mfano, hapa nilipo, nimevaa hii t-shirt. Na kama ambavyo mtaiona, hii t-shirt imeandikwa-SAFARI; ikiwa inaashiria kwamba...aah! inaashiria mbuga za wanyama. Kwa sababu, ukiangalia hata hapa juu, kuna wanyama mbalimbali ambao wamechorwa. Kwa mfano hapa yupo simba, kuna twiga hapa, kuna pundamilia, na wanyama wengine mbalimbali; kuna tembo, na wengineo pia. Kwa hiyo, ni kama tu alama au ishara kuweza kuutambulisha utalii wetu Tanzania katika ulimwengu. Kwamba, tunazo mbuga za wanyama ambazo ukifika Tanzania, utakuta wanyama wengi, wa kila aina na wanyama tofauti, na wanavutia, wanapendeza. Katika ulimwengu mzima kwa kweli ukienda sehemu nyingine huwezi ukakuta wanyama kama ambao wako Tanzania. Tanzania tuna wanyama wazuri, wengi na tuna mbuga nyingi za wanyama na zinapendeza. Na kama nilivyosema, tunautangaza utalii wetu hata kaatika mavazi tunayoyavaa. Kwa mfano hapa hii ni t-shirt, na kama ambavyo mliona ile t-shirt nyingine ambayo Happy alikuwa ameivaa. Ilikuwa ina shanga. Lakini hii pia ni t-shirt ambayo pia haina shanga lakini pia bado tunaendelea kuutaangaza utalii. Na t-shirt kama hii wanaweza wakavaa..mtu wa aina yeyote. Wanaweza wakavaa wanaume, wanaweza wakavaa wanawake, hata watoto pia, kuna t-shirt za watoto ambazo watoto wanavaa. Na, mara nyingi sana watalii wanapokuja Tanzania wanapenda sana kununua mavazi kama haya ambayo yanaashiria aah!mbuga za wanyama. Utakuta nyingine zimeandikwa-Karibu Tanzania, zingine-Uzuri wa Tanzania, na maandishi mbalimbali ambayo yanaelezea uzuri ulioko Tanzania; katika aah! Katika suala zima la utalii. Kwa hiyo, t-

shirt kama hii unaweza ukavaa mahali popote. Unaweza ukavaa nyumbani, unaweza ukavaa kazini, unaweza ukavaa sehemu yoyote ile. Kwa hiyo, hili pia ni moja ya vazi tulilo nalo Tanzania.

English translation:

Upendo: I would like to talk about tourism in Tanzania. Our tourism industry has a wide range of offerings. We have many national parks in Tanzania. For example, we have the Serengeti National Park, Manyara National Park, Tarangire National Park, Mikumi National Park, and many more. We advertise our national parks through radios, television, and the internet. We also advertise our national parks through the clothes we wear. For example, the t-shirt that I am wearing has the word SAFARI. This relays the message being on SAFARI, where you will be able to see different animals in our national parks. As you can see, in the front of this t-shirt, there are different kinds of animals. There is a lion, a giraffe, a zebra, an elephant, and other animals. This sends a message to the world that Tanzania has different and beautiful animals in our national parks. This attracts people from around the whole world. In other places, there are other animals but not such beautiful animals as those found in Tanzania. This type of T-shirt can be worn by anyone - women and men. We also have small T-shirts for kids. We have different types of T-shirts. The one worn by Happy has some beads and other decorations on it. They all advertise our natural resources. When tourists come to Tanzania, they love to wear these T-shirts which describe wild animals and other attractions in Tanzania. Some T-shirts have words like "Welcome to Tanzania." Others have inscription like "The Beauty of Tanzania," and other words which describe Tanzania. You can wear a T-shirt like this at home, at work and or anywhere. This also is one of the outfits we have in Tanzania.

About CultureTalk: CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.

© 2003-2008 Five College Center for the Study of World Languages and Five Colleges, Incorporated